

CHUO KIKUU ARDHI



TAARIFA KWA UMMA

Vyuo Vikuu Kumi na Viwili vya Afrika Vyazindua Mafunzo ya Mbinu za Namna ya Kutathmini Athari zitokanazo na Maafa

Kutokana na mahitaji makubwa ya kuwa na ujuzi wa kujiandaa na kasi ya mabadiliko ya athari zitokanazo na maafa, PERIPERI U ambayo ni ushirikiano wa vyuo vikuu kumi na viwili vya Afrika, vitazindua mafunzo ya mbinu za namna ya kutathmini athari zitokanazo na Maafa (*Risk Methods School*). Mafunzo haya ni ya kwanza ya aina yake barani Afrika yatakayofanyika kuanzia tarehe 10 mpaka 21 Septemba 2018, Chuo Kikuu Ardhi, Dar es Salaam, Tanzania.

Ushirikiano huu ni wa aina yake unaoshirikisha wakufunzi kutoka mashirika ya Umoja wa Mataifa na vyuo vikuu sita kutoka nchi mbalimbali barani Afrika. Pia, ushirikiano huu unakusudia kuongeza kasi ya makubaliano ya pamoja ya kimtizamo kati ya taasisi za elimu ya juu barani Afrika na jumuiya za kimataifa juu ya namna yakukabiliana na athari za maafa.

Mafunzo haya pia yameandaliwa ilikukabiliana na kasi ya mabadiliko ya athari za maafa zinazotokana na ukuaji holela wa miji eneo la Afrika Mashariki. Ukuaji huu wa miji una mahusiano ya moja kwa moja na ongezeko la athari za maafa yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi. Mabadiliko haya yanahitaji mbinu mpya za kisayansi ambazo ni jumuiishi, na zinazoweza kukabiliana na maafa yanayoweza kutokea mbeleni.

Mafunzo hayo ya kina yatakuwa na mada mbalimbali katika maeneo saba. Maeneo hayo ni kama vile; Athari za Maafa Mijini, Matumizi ya Mifumo ya Taarifa za Kijiografia (GIS) ya kukabiliana na maafa, Athari za Maafa kwenye sekta ya Afya, na Namna ya Kubaini Athari za Maafa ilikuboresha uwezo wa wataalam wa fani mbalimbali za maafa. Mafunzo haya yatahudhuliwa na washiriki wapatao 38 kutoka nchi kumi na moja, tisa kati ya hizo zikiwa ni kutoka Bara la Afrika. Washiriki hao wanajumuisha wanafunzi wa shahada za uzamili na uzamivu pamoja na watendaji wanaotaka kuimarisha ujuzi wa kukabiliana na maafa na kufanya tafiti zinazohusu masuala ya maafa.

Jitihada hizi zimedhaminiwa na Watu wa Marekani (USAID/OFDA), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Afya Duniani (WHO), Ushirikiano mpya wa maendeleo wa nchi za kusini mwa Afrika kuhusu maswala ya maji wa Umoja wa Afrika (*The African Union/New Partnership for Africa's Development's Southern African Network of Water Centres of Excellence (AU/NEPAD SANWATCE)*), na Chuo

Kikuu cha Stellenbosch – kituo cha mafunzo ya elimu ya juu cha Afrika (Stellenbosch University's Africa Centre for Scholarship.)

Mafunzo mengine kama haya yataandaliwa na Chuo Kikuu cha Gaston Berger, St. Louis, Senegal mnamo Februari 2019.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na **Alberto Francioli:** albertofrancioli@sun.ac.za (Mobile: +27 84 208 1870) au **Benedict Malele:** benedictmalele@yahoo.com (Mobile: +255754 980 872)

Imetolewa na
Ofisi ya Uhusiano



PERIPERI U

PARTNERS ENHANCING RESILIENCE
FOR PEOPLE EXPOSED TO RISKS



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE



**World Health
Organization**